# DAFTARI LA MKUTANO MKUU

**JIWEKE TAYARI!**

Kabla ya kuanza kwa mkutano, unaweza kujiandaa kusikia sauti ya Bwana kwa kutafuta ufunuo wako binafsi.

- ◯ Je, Nimechukua muda kusali sala binafsi?
- ◯ Je, Nimesoma maandiko yangu?

"Ninakualikeni kusikiliza vitu vitatu wakati wa mkutano huu: ukweli halisi, mafundisho halisi ya Kristo, na ufunuo halisi. . . . Ninaweza kukuhakikishieni kwamba mtakachokisia leo na kesho kinabeba ukweli halisi."

*Rais Russell M. Nelson*[1]

# ULIZA,

"Ufunuo karibia daima huja kama jibu la swali."

*Mzee Jeffrey R. Holland*[2]

## na Kisha Sikiliza

"Ufunuo halisi kwa ajili ya maswali ndani ya moyo wako utafanya mkutano huu kuwa wenye thawabu na usiosahaulika." Kama bado hujatafuta kutumikiwa na Roho Mtakatifu ili akusaidie kusikia kile Bwana angetaka wewe usikie katika siku hizi mbili, nawaalika kufanya hivyo sasa.

*Rais Russell M. Nelson*[3]

### Unawaza nini akilini mwako?

Fikiria kuhusu maswali, au dukuduku ambayo yawezekana kuwa unayo? Unaweza kuandika chini hapa na kuyaweka akilini unapokuwa unasikiliza mkutano. Hata kama utakuwa huna kitu maalumu akilini mwako, Bwana atakusaidia kupata njia ya kujifunza na kukua unapofanya jitihada ya kumsikiliza Yeye.

Hapa kuna baadhi ya mifano na nafasi kuandika ya kwako:



# ANDIKA!

Mwonyeshe Bwana kuwa uko tayari kupokea na kufanyia kazi ufunuo kwa kufokasi katika kumsikiliza Roho na kuandika kile unachofikiria na kuhisi. Usijali kuhusu kuandika kila kitu kidogo kinachosemwa. Unaweza daima kurudi na kusoma au kutazama mahubiri haya baadaye.

"Kuna mfanano mkubwa [wa kuchukua taarifa kwa kuandika] katika Kitabu cha Mormoni. Kuna yale mabamba makubwa, ambayo yana historia ya watu, na mabamba madogo, ambayo ni mafunuo na maandishi matakatifu. Kama mtu anasikiliza mahubiri . . . na anaandika chini kile mtu anachoongea, huyu anaandika kwenye mabamba makubwa—hii ni historia ya mkutano. Kama unaandika ushawishi binafsi ambao unakuja kwako kwa njia ya Roho Mtakatifu, wewe unatengeneza mabamba madogo yako mwenyewe."

*Mzee David A. Bednar*[4]

Walichofundisha:

Hisia Zangu na Misukumo:

**MSIKILIZE ROHO. UNAHISI NINI?**

"Kama chote tunachopokea ni kile tu mwalimu anachowasilisha, tunakosa kile kilicho cha muhimu zaidi."


*Mzee David A. Bednar*[5]

Walichofundisha:



**HAKUNA NJIA ISIYO SAHIHI YA KUANDIKA TAARIFA**

Je, una wakati mgumu kufokasi? Jaribu kuifanya taarifa hiyo kama yako wewe binafsi. Ongeza michoro fulani, ukiumba herufi, au vielelezo ili ikusaidie kukumbuka hadithi, nukuu, au ushawishi ambavyo vina maana fulani kwako.



## Hisia Zangu na Misukumo:

**TUA!**

Je! Umepokea majibu yo yote ya maswali yako hadi sasa? Ikiwa ndivyo, chukua muda kuandika mwongozo na maelekezo ambayo umepokea.

"Naahidi kwamba unapoisikiliza sauti ya Bwana kwako katika mafundisho ya mkutano huu, na kutenda kulingana na msukumo huo, utahisi mkono wa mbingu juu yako, na maisha yako na ya wale wanaokuzunguka yatabarikiwa."

*Mzee Neil L. Andersen*[6]

"Katika maneno hayo mawili—"Msikilize Yeye"—Mungu anatupatia mpangilio wa mafanikio, furaha, na shangwe katika maisha haya. Inatubidi *kusikiliza* maneno ya Bwana, *kuyatii* hayo, na *kufuata* kile Alichotuambia!"

*Rais Russell M. Nelson*[7]

Walichofundisha:

Hisia Zangu na Misukumo:

# SASA NINI KINAFUATA?

Mara mkutano unapokuwa umekwisha, ni wakati wa kufanyia kazi mambo yale uliyoyasikia na kuhisi. Hapa kuna baadhi ya maswali ya kukuwezesha kuanza:

- Je, Ni kitu gani kimoja ninachoweza kufokasi juu yake wakati ninaposonga mbele?
- Je, kuna kitu cho chote kuhusu maisha yangu ambacho ninasukumwa kubadilika?
- Ni misukumo gani nitakayoifanyia kazi?
- Je, Nilimsikilizaje Yeye wakati wa mkutano?
- Je, Ninawezaje Kumsikiliza Yeye vizuri zaidi katika maisha yangu ya kila siku?

Je, umesisimka na njia ambayo taarifa zako za mkutano ulizoandika zilivyofika pamoja? Je, unayo michoro au vielelezo ambavyo vimestahili- papo hapo? Shiriki pamoja nasi! Tuma picha ya taarifa zako kwa barua pepe kwenda kwa ftsoy@ChurchofJesusChrist.org au ziweke kwenye Instagram na tag @strivetobe page!

“Majibu ya sala zako maalum yanaweza kutoka moja kwa moja kutoka kwenye hotuba fulani au kutoka kwenye kifungu fulani. . . . Nia ya dhati ya kutaka kusikia na kufuata maneno ya ushauri itatayarisha njia kwa ajili ya ufunuo binafsi.”

*Mzee Dieter F. Uchtdorf*[8]

**JE, UNAHITAJI NAKALA ZAIDI?**
Pakua na uchapishe daftari hili kwenye **conference.ChurchofJesusChrist.org**.


**Muhtasari**

1. Russell M. Nelson, “Ukweli Halisi, Mafundisho Halisi, na Ufunuo Halisi,” mkutano mkuu wa Okt. 2021 (*Ensign* au *Liahona*, Nov. 2021, 6).
2. Jeffrey R. Holland, “Cast Not Away Therefore Your Confidence,” *Ensign*, Machi 2000, 9.
3. Russell M. Nelson, “Ukweli halisi, Mafundisho Halisi na Ufunuo Halisi,” *Liahona*, Nov. -7, 6–7.
4. David A. Bednar, “Create Your Own Small Plates” (video), Churchof JesusChrist.org.
5. David A. Bednar, “Tengeneza Mabamba Madogo Yako Wewe Mwenyewe.”
6. Neil L. Andersen, mkutano mkuu wa Okt. 2017 (*Ensign* au *Liahona,* Nov. 2017, 126).
7. Russell M. Nelson, “Msikilize Yeye,” mkutano mkuu Apr. 2020 (*Ensign* au *Liahona*, Mei 2020, 89).
8. Dieter F. Uchtdorf, “Mkutano Mkuu—Hakuna Baraka za Kawaida,” *Ensign* au *Liahona*, Sept. 2011, 4.



© 2022 na Intellectual Reserve, Inc.
Haki zote zimehifadhiwa.

IDHINI YA KUCHAPISHA UPYA KIJITABU HIKI IMETOLEWA KWA MATUMIZI BINAFSI, YASIYO YA KIBIASHARA. HII INAJUMUISHA IDHINI KWA VIONGOZI WA KATA KUCHAPISHA IDADI NDOGO YA NAKALA KWA AJILI YA WALE WANAOWAHUDUMIA KATIKA NAFASI ZA MIITO YAO. VIJITABU SHARTI VICHAPISHWE KWA UKAMILIFU WAKE. HII HAIJUMUISHI IDHINI YA KUVIWEKA MTANDAONI, KUTUMIA TENA AU KUSAMBAZA NYENZO HII. MATUMIZI YO YOTE YA ZIADA YA NYENZO HII YANAHITAJI KUIDHINISHWA.

**permissions.ChurchofJesusChrist.org**


KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO